**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule: 0767487425**

**Makamu M/Shule: 0625977132**

**Matron/Patron: 0613537212**

**Shule ya Sekondari Bitale,**

**S.L.P 82, KIGOMA.**

**Tarehe ……………….**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BITALE, HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA, MKOA WA KIGOMA MWAKA …………………..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ………….. katika tahasusi ya EGM,HGE, KLF

Shule ya Sekondari ya Bitale ipo katika Kijiji cha Bitale umbali wa Kilometa 20 Kutoka kigoma mjini. Hivyo mzazi au mlezi unatakiwa kumpandisha mwanao katika magari yaendayo kigoma mjini na mwanafunzi atashuka Kituo cha mabasi ya mikoa yaani Kigoma stendi mpya. Mwanafunzi akifika stendi mpya Kigoma atapanda daladala ziendazo bitale hadi mkongoro kwa Tsh 1000 mpaka stendi ya Bitale. Akifika stend atatembea kwa umbalu wa mita 300 kuingia eneo la shule ya sekondari bitale.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ……………….. hivyo mwanafunzi anatakiwa afike shuleni mapema.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili(2) ndefu zinazofika kwenye kisigino, rangi ni ORANGE, kitambaa ni cotton 100%. Mshono wa sketi ni wa kawaida rinda kumi. Kitambaa cha sketi kiwe rangi kama inavyoonekana katika picha ukurasa wa mwisho.

ii. Mashati mawili yenye kola (cotton 100%) rangi nyeupe mikono mirefu. Rangi ya Hijab (Juba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.Shati iwe mikono mirefu rangi nyeupe. Wakati wa kazi mwanafunzi avae hijabu rangi ya kijivu pamoja na shamba dress. Hivyo, mzazi unatakiwa kumshonea mwanao hijabu rangi mbili( nyeupe na kijivu).

iii. Sare ya Michezo ni track suit pair 2 za rangi ya blue yenye michirizi myeupe.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;
vi. Sweta moja yangi ugoro mikono mirefu yenye shingo ya V.
vii. Nguo za kushindia (shamba dress) au gauni mbili (2) za heshima zinazovuka magoti zenye rangi ya darkblue kitambaa kizito yenye marinda makubwa, kola ya round, mikono mifupi isiyoonesha kwapa.
viii. Tai mbili(2) za rangi inayofanana na sketi.
ix. T-shirt mbili(2) zenye kola (fom 6) rangi ya Blue bahari.

- **Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**
  - Daftari za 10 za counter Quire 3.
  - **Ream (A4)** za Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;(DOUBLE A)
  - Vitabu vya masomo ya tahasusi husika angalau kitabu cha ziada kimoja kwa kila somo (reference book).
  - Scientific Calculator na Mathematical set kwa wanafunzi wa (EGM)
  - File folder moja la kawaida.
  - Godoro kwa wanafunzi wa Bweni size liwe 2.5ftx6ft
  - Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki, blanket 1, foronya ya godoro 1, mto na chandarua kimoja rangi ya pinki pembe nne .
  - Nguo za ndani za kutosha;.
  - Taulo kubwa la kujifutia.
  - Kandambili kwa ajili ya kuogea.
  - Raba nyeusi kwa ajili ya michezo.
  - Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).

- Ndoo 2 ndogo (lita kumi) zenye mifuniko;
- Mwanafunzi aje na Kwanja au fyekeo, Soft broom na hard broom
- Wanafunzi wa KLF waje na majembe.
- Wanafiunzi wa EGM waje na reki, Panga na Squizer.
- Wanafunzi wa HGE waje na mifagio ya nje na mopper..
- Wanafunzi wa KLF waje na brush za kusugulia masinki ya chooni.
- Tranka kwa ajili ya kuewekea vitu vyake.
- Aje na Pocket money kwa ajili ya kununua mahitaji yake.
- Mahitaji mengine kama sabuni za kuogea,kufulia na mafuta ya kujipakaa, dawa ya meno, taulo za kike (Pedi) n.k

**ANGALIZO**

Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine yeyote zaidi ya zilizoainishwa. Aidha wakati wa kuripoti mwanafunzi afike shule akiwa amevaa track suit ya Blue yenye michirizi myeupe.

**MICHANGO MBALIMBALI**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000** |

Fedha hii ilipwe kupitia Benki ya NMB namba **51601100028 Ji**na la akaunti ni **BITALE SECONDARY SCHOOL.** Fedha hii ilipwe kwenye akaunti ya shule kuanzia tarehe 01.07.2026 na mwanafunzi afike shuleni na BPS ya Benki na kamwe mwanafunzi asifike na fedha taslimu ‘ cash’ shuleni.

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na

utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni:

i. Wizi

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafukwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

viii. Uvutaji wa sigara;

ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

I. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
II. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
III. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
IV. Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mawanafunzi waoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII



JEREMIA MGASA PETER
MKUU WA SHULE

**The Headmaster**
**Bitale Secondary School**
**14 APRIL 2026**
**P.O.Box 82**
**Kigoma**

NB. Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama Walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ni Mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MAWANAFUNZI AU MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE , NI VYEMA KUWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA KUPIGA NAMBA 0767487425 AU 0625977132.

**HALMSASHAURI YA WILAYAN YA KIGOMA**
**SHULE YA SEKONDARI BITALE**
**FOMU NAMBA 01.**

## HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi ……………………………………………………………………
2. Jina la baba …………………………………………………………………………..
3. Jina la mama ……………………………………………………………………………
4. Jina kamili la Mlezi…………………………………………………………………….
5. Anuani ya Mzazi/Mlezi ………………………………………………………………….
6. Uhusiano wa Mlezi ……………………………………………………………………
7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi) …………………………….....
8. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni ……………………………………
9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni …………………………………………
10. Kama ni mfanyakazi, kazi yake ni ……………………………………………………
11. Afya ya mwanafunzi; kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum, tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi………………………
12. Madhehebu ya dini ……………………………………………………………………..
13. Jamaa na ndugu wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi

| | JINA KAMILI | KAZI YAKE | NAMBA YA SIMU | |
|---|---|---|---|---|
| (a) | …………………………… | ……………………… | ………………….... | Bandika picha |
| (b) | …………………………… | …………………….. | …………………… | Bandika picha |
| (c) | ………………………………... | ……………………… | ………………… | Bandika picha |

(d) ………………………………… ……………………….. ………………... 

| Bandika picha |
|---|

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA**

**SHULE YA SEKONDARI BITALE**

FOMU NA. 2

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Jina la mwanafunzi.......................................................................................................

Jinalamzazi/mlezi………………………………………………………………………...

Anuani ya mzazi/mlezi ………………………………………………………………

Uhusiano………………………………………………………………………………..

Mimi .......................................................................................nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Bitale naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Hivyo naahidi kuwa, nitajibidisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi.

Ili kutimiza shabaha hiyo, **ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA KUTII kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria.** Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Saini ya mwanafunzi …………………………………Tarehe…………………….

---

Mimi ………………………………………………… mzazi/mlezi……………………………… ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na uongozi wa shule.

Saini ya mzazi/mlezi........................................................ Tarehe..........………...................

KIGOMA DISTRICT COUNCIL
BITALE SECONDARY SCHOOL
SLP 82, KIGOMA
FORM NAMBER 03
MEDICAL EXAMINATION FORM

To medical Officer I/C of ........................................................................................Designated Hospital, P.O. Box .................................................................................................... Please examine the above named in full as to his/her physical and mental fitness for being able to pursue two years of secondary school education. The examination should include categories a-m.

In case of any acute or defect/disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs.

(a) Pupil's name ………………………………………………………………………

(b) Age ………………………………………………………………..…………….

(c) Stool test ………………………………………………………………………...

(d) Blood group ………………………………………………………………………

(e) Urine analysis …………………..…………………………………………………

(f) Sphills test ………………………………………………………………………….. (g) Chest test ………………………………………………………………………… (h) Speech ……………………………………………………………………………. (i) Eye test …………………………………………………………………………

(j) Abdomen ……………………………………………………………………………

(k) Chest X-ray ………………………………………………………………………..

(l) Sickle cell test ………..……………………………………………………………

(m) WCB total Differential ........................................................................

Addition information and physical defect or impairment to pursue further studies
………………………………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………….

Signed by…………………. Designation …………………………………...........

**Official Stamp**

**Date:**

**KIAMBATISHO CHA RANGI YA SARE ZA SHULE**



**RANGI YA SKETI ORANGE**



**SHAMBA DRESS DARK BLUE**



**TSHIRT BLUE**




**SHUKA PINK**